

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA
FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021**

**SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA
S.L.P 737
Simu: 0755279058
SUMBAWANGA.
14/12/2020.**

Kumb. No. SUSS/J/VOL 2/13

KWA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari kidato cha Kwanza mwaka 2021 baada ya kumaliza Elimu yako ya Shule ya Msingi HONGERA SANA. Wewe umepangiwa Shule ya Sumbawanga Sekondari iliyopo Manispaa ya Sumbawanga baada ya kupita viwanja vya Sabasaba ukitokea mjini.

Utatakiwa kuripoti shule siku ya 04/01/2021 bila kukosa tayari kwa kuanza masomo. Ukichelewa nafasi yako inaweza kuchukuliwa na mtu mwingine.

**YAFUATAYO NI MAAGIZO AMBAYO UTATAKIWA KUYATIMIZA
KABLA HAUJAJIUNGA NA SHULE HII**

A. SARE YA SHULE (WAVULANA)

1. WAVULANA

- a) Mashati meupe ya tetron mikono mifupi mawili (2)
- b) Suruali mbili, moja **kijani nyeusi** na **Bluu bahari**. (ziwe na rinda mbili mbele na chini turn-up)
- c) Viatu jozi mbili vya ngozi nyeusi vyenye visigino vifupi na vyenye kamba
- d) Socks /Stocking jozi mbili nyeusi
- f) Raba jozi moja kwaajili ya michezo
- g) Sweta la Bluu kwaajili ya kujikinga na baridi
- h) Tracksuit nyeusi kwaajili ya michezo
- k) Mkanda mweusi wa ngozi

2. WASICHANA

- a) Mashati meupe ya tetron mikono mifupi mawili (2)
- b) Sketi mbili, moja **kijani nyeusi** na **Bluu bahari**.
- c) Viatu jozi mbili vya ngozi nyeusi vyenye visigino vifupi na vyenye kamba
- d) Socks /Stocking jozi mbili nyeupe
- f) Raba jozi moja kwaajili ya michezo
- g) Sweta la Bluu kwaajili ya kujikinga na baridi
- h) Tracksuit nyeusi kwaajili ya michezo

B. VIFAA VYA DARASANI

- a) Daftari (Counter books 12)
- b) Mathematical set (Mkebe)
- c) Mkoba(begi) mweusi wa kubebea daftari

C. VIFAA VYA USAFI

- i) Jembe jipya na mpini wake
- ii) Ndoo ndogo ujazo wa lita 10
- iii) Fyekeo 1
- iv) Ufagio la chelewa lenye mpini

NB: Pia mwanafunzi aje na miche miwili (2) ya miti kati yake mmoja uwe wa matunda.

MZAZI MWANDALIE MWANAO MAHITAJI YA SHULE MAPEMA ILI AANZE MASOMO YAKE KWA WAKATI.

D. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo utafafanuliwa na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
- c) Kutimiza maandalizi ya jioni kwa makini.
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa wa mwili na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote wa madarasa na unapotoka nje ya shule.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

E. MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

- 1. Wizi.
- 2. Uasherati na ushoga.
- 3. Ubakaji.
- 4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, Uvutaji bangi, Cocane, Mirungi, Kubeli NK.
- 5. Kupigana au Kupiga.
- 6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- 7. Kudharau bendera ya Taifa.
- 8. Kuo au kuolewa.
- 9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- 10. Kutoa mimba
- 11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- 12. Kukataa kwa makusudi adhabu.
- 13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
- 14. Kukataa kwa makusudi kufanya mitihani ya ndani na nje ya shule.
- 15. Kufuga ndevu.
- 16. kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- 17. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo hayo na kuyatekeleza kwa ukamilifu

**KARIBU SANA SUMBAWANGA SEKONDARI
WAKO KATIKA UJENZI WA TAIFA**

.....
**MASAWA, K.
MKUU WA SHULE**